International Resources Group

IRG is ISO 14001 Certified

Tathmini Mkakati wa Mazingira, Kisiwa cha Mafia, Muhtasari Sera Na 1
Muhtasari umeandaliwa na International Resource Group, Washington, DC naTaasisi ya Kutathimini Rasilimali Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Kilindoni, Mafia Distict © H. Sosovele (2008)

MIPANGO MIZURI NA UTARATIBU IMARA WA USIMAMIZI WA RASILIMALI NI MUHIMU KWA MAENDELEO YA KISIWA CHA MAFIA

Mafia Airport, B Thiam (2008)

Umetayarishwa kwa ajili ya Mpango wa Changamoto za Milenia -Tanzania (Februari 2009)

Tathmini Mkakati wa Mazingira, Kisiwa cha Mafia, Muhtasari Sera Na 1
Muhtasari umeandaliwa na International Resource Group, Washington, DC na Taasisi ya Kutathimini Rasilimali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

MIPANGO MIZURI NA UTARATIBU IMARA WA USIMAMIZI WA RASILIMALI NI MUHIMU KWA MAENDELEO YA KISIWA CHA MAFIA

UTANGULIZI

Aliyekuwa Rais wa Marekani Bwana George W. Bush na Rais wa Tanzania Jakaya Kikwete walitiliana saini makubaliano ya kutekeleza Mpango wa Changamoto za Milenia utakaogharimu Dola za Kimarekani milioni 698.1. Lengo kuu la Mpango huu ni kupunguza umasikini kwa kuongeza ukuaji wa uchumi, kuongeza kipato ngazi ya kaya, na kupandisha ubora wa maisha kupitia uwekezaji katika miundombinu mbalimbali. Miradi itakayozingatiwa katika makubaliano haya ni pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege na barabara, upatikanaji wa nishati (umeme)) na usambazaji maji safi na salama.. Miradi hii inatarajiwa kuwasaidia Watanzania kupata nishati bora, usafiri mzuri na maji safi na salama ambavyo vitainua ubora wa maisha yao.

Kisiwa cha Mafia kina utajiri mkubwa wa bioanuai kama vile aina mbalimbali za samaki, pweza na ngisi. Uvuvi ni shughuli kuu ya kiuchumi kwa wakazi wa Mafia na maeneo jirani. Hata hivyo aina zote za samaki mbali na ngisi zimevuliwa kupita

kiasi na sasa hivi hazipatikani kwa urahisi. Kisiwa cha Mafia pia kina utajiri wa wanyama pori kwa mfano aina za vyura na mijusi inayopatikana Mafia tu; popo wakubwa wanaioshi kwenye mapango. Rasilimali nyingie muhimu kwa Mafia ni ardhi, watu, maeneo ya kihistoria ambavyo

vyote ni muhimu katika kukuza utalii wa Mafia

Kisiwa cha Mafia kimeanza kuwa kivutio kikubwa cha utalii, kwa kuhudumia soko la kimataifa kwa kuunganisha watalii wanaokwenda Mafia na Zanzibar, Rufiji, Pori la Akiba la Selous kwa kusini ya Tanzania na Ngorongoro, Serengeti, na Mlima Kilimaajaro kwa sehemu za kaskazini. Idadi ya ndege, abiria na mizigo kwenda au kutoka Mafia imeongezeka tangia mwaka 1999 na inatarajiwa kuongezeka zaidi kufikia mwaka 2030 hadi kilogramu milioni 1.4 za mizigo na abiria wapatao. 180,000.[1] Mafia inaanza kuwa maarufu katika masuala ya nishati kimataifa kutokana na utafutaji wa gesi eneo la Ndagoni.

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA

Njia kuu za usafiri kwenda na kutoka Mafia zimekuwa ni kwa bahari au kwe ndege – kwa watu wachache wanaomudu gharama za ndege. Sehemu ya tatizo la maendeleo kwa Mafia ni miundombinu mibovu ya usafiri na uchukuzi ambayo imewasabibishia wakazi wa Mafia kukosa fursa za kuleta maendeleo. Wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu wamesita kwenda Mafia kwa kuhofia usafiri duni. Mafia yenyewe ni mkusanyiko wa visiwa vidogo

[1] Makadirio haya yalifanywa kabla ya kutokea kwa tatizo la kuporomoka kwa uchumi duniani, ambapo inasemekana idadi ya watalii watakaokuja Tanzania inaweza kupungua.

vidogo vinane, lakini ni visiwa vitano tu vinavyokaliwa na watu.

Mpango wa uboreshaji wa uwanja wa ndege na matengenezo yake katika sehemu mbalimbali na shughuli nyingine za ujenzi na uchumi zitakazotokana na upanuzi wa uwanja wa ndege vinaweza kuleta faida au madhara katika uchumi wa Mafia na Taifa, na hata kusababisha uharibifu wa mazingira ya Mafia.

Ni katika hali hii Serikali ya Tanzania kupitia Mpango wa Changamoto za Milenia-Tanzania waliamua kufanyika kwa Tathmini ya Mkakati ya Mazingira kwa Mafia ili kuona mambo ambayo yatahitaji uamuzi wa kisera. Lengo la tathmini hii ni kushauri mfumo wa upangaji na usimamizi wa Rasilimali za Mafia na kuanisha vipaumbele ambavyo serikali na Mradi wa Milenia watavifanyia kazi. Baadhi ya mabadiliko yatakayotokana na kuongezeka kwa shughuli za uchumi kwa ujumla yataathiri utalii. Tathmini hiyo pia ilizingatia na kupendekeza kiwango cha juu cha uhimilivu kinachoweza kutumika katika shughuli za utalii. Kiwango hicho kikipitiliza, basi mazingira yatakuwa hatarini. Kwa mfano, uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Mafia ulikusudia kuhudumia wasafiri 100 kwa saa.moja Hali hii itachangia kwa kiwango kikubwa uharibifu wa mazingira kwa kuongeza idadi ya watu na mahitaji katika rasilimali. Bila kuwa na mipango madhubuti ya usimamizi wa rasilimali, shughuli hizi za maendeleo zitakazotokana na uboreshaji wa uwanja wa ndege zinaweza kuleta madhara zaidi na kusababisha mabadiliko ya muda mrefu katika rasilimali na kwa hali hiyo kuongeza kasi ya kukua kwa umasikini. Kwa hiyo, kupunguza idadi ya wageni kwa saa au siku linakuwa ni suala la kisera ambalo ni budi lichukuliwe ili kunusuru mazingira ya Mafia.

Katika hali ya usimamizi duni na uratibu mbovu wa shughuli za maendeleo Mafia, ni dhahiri kuwa masuala ya kijamii na kiuchumi yanayotokana na ujenzi wa uwanja wa ndege yatakuwa na walakini endapo serikali haitachukua hatua za haraka kuwekeza katika kuboresha utayarishaji na usimamizi wa mipango mbalimbali ya maendeleo kwa Kisiwa cha Mafia. Serikali Kuu ni lazima iweke kipaumbele na kuwezesha kiufundi na kifedha utayarishaji wa mapendekezo yafuatayo:

MAPENDEKEZO YA KISERA

1. *HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA IBORESHE UTAWALA BORA*

Baadhi ya changamoto zinazoikabili Mafia, zinatokana na hitilafu katika masuala ya utawala bora na usimamizi wa majukumu yake yenyewe. Uongozi wa Wilaya ni lazima uhakikishe kunakuwepo na ushirikishwaji wa kutosha, uwazi, na uwajibikaji kwa wananchi. Watumishi wa Halmashauri watekeleze majukumu yao ipasavyo. Halmashauri inashauriwa ifanye yafuatayo katika kuimarisha utawala bora.

- Kuanzisha na kuimarisha Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Mazingira kwa Wilaya ya Mafia na kuhakikisha mazingira yanazingatiwa katika mipango yote ya Wilaya na kati ya wilaya na serikali kuu.
- Kuanzisha na kuzisimamia sheria ndogo zinazolinda mazingira
- Kutayarisha na kutekeleza *Mpango wa Uboreshaji wa Uwezo wa Watendaji* katika wilaya na hasa Idara ya Mipango, Kamati ya Fedha, katika utayarishaji na usimamizi wa mipango ya maendelo endelevu
- Wilaya ihakikishe kuna ushirikishwaji wa kutosha kwa wananchi wa kawaida bila kujali jinsia, dini au umri wao katika

kupanga na kusimamia shughuli za maendeleo

- Wilaya itayarishe na kutekeleza *Mpango wa Uhamasishaji kwa Wananchi* ili wawe tayari kukabiliana na chnagmoto za maendeleo zinazotokana na uboreshaji wa uwanja wa ndege
- Wilaya izingatie na kutatua matatizo ya kijamii, kimila, kitaasisi na kifedha ambayo yamekuwa ni kikwazo kwa wananchi wa Mafia kwa muda mrefu. Hii itawapa wananchi fursa ya kuwa sehemu ya mabadiliko yanayokusudiwa.

2. WILAYA IANZISHE UTAYARISHAJI WA MIPANGO MBALIMBALI

Uboreshaji wa uwanja wa ndege na shughuli zitakazofuatia kutokana na hali hiyo zinaweza kusababisha mabadiliko makubwa ya namna rasilimali zinavyotumika Mafia. Ni lazima kwa hiyo, kuandaa mipango mbalimbali ya matumizi ya rasilimali ili kuratibu, kusimamia na kuelekeza namna rasilimali hizo zinavyoweza kutumika. Mipango ifuatayo ni budi itayarishwe mapema iwezekavyo.

- Halmashauri ya Mafia itayarishe Mpango Kabambe wa Matumizi ya Ardhi
  - Wilaya isiruhusu wawekezaji kununua ardhi moja kwa moja toka kwa wananchi. Wawekezaji wote wapatiwe ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania
  - Wilaya isiruhusu wananchi kuuza maeneo yao kwa wawekezaji badala yake wahimizwe kuingia ubia na wawekezaji hao. Kwa kufaya hivyo watakuwa wanatekeleza mpango wa **MKURABITA.**
- Wizara ya Mali Asili na Utalii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia watayarishe na kutekeleza *Mpango Kabambe wa Utalii kwa Mafia.* Mpango huu utokane na viwango vya uhimilivu na vile vinavyo onesha ukomo katika matumizi.
- Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania na Halmashuri ya Wilaya ya Mafia, watayarishe na kutekeleza *Mpango Kabambe wa Gati* zitakazounganisha gati za Mafia, Kilwa, Rufiji na Mkuranga.
- Halmashauri ya Wilaya ya Mafia itayarishe na kusimamia *Mpango Kabambe wa Ukusanyaji na, Uteketezaji wa Taka Ngumu na Laini.* Mpango huu uainishe maeneo muhimu ya kukusanya, kuchambua, kutupa na kuteketeza taka za aina mbalimbali. Mpango utoe motisha kwa wananchi watakaochukua hatua za makusudi za kupunguza uzalishaji na utupaji ovyo wa taka.
- Tathmini ya Athari za Mazingira na Tathmini nyingine zitakazotokana na miradi na programu hii zifanywe katika kila sehemu husika. Ili hili lifanyike, hapana budi kuwa na mipango ya kujenga uwezo kwa watendaji wa wilayani. Miradi na programu zote zitakazofanyika Mafia ni budi zizingatie agizo la Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

3. HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA IFUATILIE NA IPUNGUZE MADHARA YA MAZINGIRA YANAYOTOKANA NA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Maeneo ya kuzingatiwa ni haya yafuatayo:

- ***Maji*** **.** Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Kushirikiana na Halmashauri ya Mafia wafanye tathmini ya vyavyo vya maji vya ardhini ili kubaini kiasi na ubora wa maji uliopo kabla miradi mikubwa ya maendeleo haijaanza. Kigezo muhimu katika kuamua idadi na ukubwa wa hoteli, viwanda au miradi

mingine itakayoendelezwa Mafia kiwe ni upataikanaji wa uhakika wa maji safi na salama.

  - Shughuli zote za maendeleo budi zitumie njia mbadala za kupunguza matumizi makubwa ya maji

  - Halmashauri itoe kipaumbele katika kusambaza maji kwa wananchi wote na hasa katika visiwa vidogo ambako maji ni adimu

- ***Nishati:*** Matumizi ya mkaa yasiruhusiwe:

  - Miradi mipya ya utalii ni lazima itumie nishati mbadala kwa kiwango cha asilimia 50 ya mahitaji yao yote ya nishati

  - Kama suluhisho la kudumu, Halmashauri na Wizara ya Nishati na Madini wafikirie kuunganisha wilaya ya Mafia katika gridi ya Taifa kupitia waya umeme za chini ya bahari.

- **Utalii:**

  - Iwekwe sheria au taratibu ya kupunguza idadi ya wageni wanaotembelea maeneno nyeti kiikolojia ili kunusuru maeneo hayo kutokana na msongamano wa watalii. Maeneo hayo ni kama ya kupiga mbizi, utamaduni na michezo ya uvuvi. Idadi inaweza kuwekwa kulingana na msimu na gharama.

  - Kupunguza idadi ya wageni watakaotumia uwanja wa ndege wa Mafia ili kupunguza haja ya kujenga mahoteli zaidi

- ***Viumbe vya Baharini***: Shughuli za maendeleo zinaweza kusababisha uharibifu mkubwa katika Hifadhi ya Bahari ya Mafia. Kwa hiyo basi:

  - Serikali Kuu ni lazima ihakikishe Hifadhi ya Bahari ya Mafia ina watumishi wa kada mbalimbali wa kutosha, vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi na inapata ruzuku ya kutosha ili iweze kukabiliana na changamozto zitakazojitokeza.

4. *HALMASHAURI ITEKELEZE SHUGHULI ZINAZOLENGA KUIMARISHA FAIDA ZA KIUCHUMI*

Shughuli za maendeleo zinazoweza kuamshwa na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia zinaweza kuwa chachu ya kukua kwa uchumi wa Mafia. Hata hivyo ili wananchi wa Mafia wanufaike na mabadiliko haya; yafuatayo ni budi yatekelezwe:

- Wananchi wahamasishwe ili waweze kutumia fursa ya ujenzi wa uwanja wa ndege kuimarisha na kuboresha uzalishaji katika sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazotakiwa katika soko la utalii. Ni budi kuongeza ubora wa bidhaa ili zipate soko.

- Kujenga Chuo cha Ufundi Stadi na kuhakikisha vijana wote wa kike na wakiume na wadini mbalimbali wanapata fursa ya kusomea stadi mbalimbali kama ujenzi, umeme, ufundi bomba, upakaji rangi, ufundi magari, useremala, ushonaji, utembezaji watalii nk. Stadi hizi zitawawezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri na kwa hiyo kunufaika kutokana na uboreshaji wa uwanja wa ndege.

- Halmashari kwa kushirikiana na mabenki na taasisi za fedha watafute jinsi ya kupata mikopo ili vijana waweze kujipatia mitaji ya kuanzisha biashara au shughuli nyinginezo

- Vikundi vidogo vya wajasiriamali vya akina mama na vijana vianzishwe na vipatiwe misaada
- Biashara ya mbata ianzishwe tena kwani inayo nafasi ya kutoa ajira kwa vijana wengi.

5. HALMASHAURI ICHUKUE HATUA KUPUNGUZA MADHARA YA KIJAMII YATAKAYOTOKANA NA SHUGHULI ZA MAENDELEO MAFIA

Shughuli za uboreshaji wa uwanja wa ndege na mipango mingine zinaweza kusababisha mabadiliko katika mahusiano ya kijamii na tamaduni katika wilaya ya Mafia. Mapendekezo yafuatayo budi yatekelezwe ili kupunguza athari za kijamii zinazoweza kujitokeza.

- Wananchi wahamasishwe na watambue madhara ya utalii na shughuli nyingine za maendeleo katika mila na desturi zao
- Utayarishwe Mwongozo utakao waongoza watalii namna ya kuishi na wenyeji huko Mafia-Mwongozo ubainishe yale yanayokubaliwa kulingana na mila na desturi za wananchi wa Mafia na yale yasiyokubaliwa huko ili watalii wasiyafanye
- Halmashuri ijenge shule nyingi zaidi za sekondari ili watoto wapate elimu. Shule hizo zipatiwe vifaa vya kisasa kama kompyuta na vinginevyo.
- Halmashauri na Wizara ya Afya waanzishe kliniki ya baharini kwa kutumia boti maalumu itakayokuwa inatoa huduma za dharura katika visiwa vidogo.
- Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ipeleke watumishi wa kutosha Mafia ili kukabiliana na changamoto za maendeleo.
- Halmashauri na Wizara ya Afya wayasaidie mashirika na vikundi vya hiyari katika kutoa elimu juu ya UKIMWI, upimaji wa UKIMWI na wajenge vituo vingi zaidi vya upimaji wa hiari.

Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ihakikishe kuwa kuna uhusiano wa karibu baina yake na Serikali Kuu na taasisi zake hasa katika kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa mipango mbalimbali. Halmashauri ya Wilaya pia ifanye kazi na Serikali Kuu katika kutafuta vyanzo vya fedha zitakazosaidia katika kusimamia na kutekeleza mipango mbalimbali iliyopendekezwa hapa. Utaratibu wa kuihusisha sekta binafsi katika ubia na wananchi au serikali uzingatiwe.